# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutanguliza shukurani zangu kwa Mwenyezi Mungu aliyetuumba, kutujaalia uhai na uzima uliotuwezesha kupata fursa hii adhimu na muhimu ya kukutana katika Mkutano huu wa Kumi na Moja kwa lengo la kuwatumikia wananchi pamoja na kutekeleza jukumu letu muhimu la kuchambua na kutafakari Programu za Fungu E04 za Bajeti ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 107, Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la Mwaka 2020).

**Mheshimiwa Spika,** kwa dhati, Kamati ya PAC inampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uamuzi wake wa busara alioufanya wa kutekeleza matakwa ya kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Uanzishwaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Namba 11 ya mwaka 2003 kwa kumteua Ndugu Said Khamis Juma kuwa Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Uamuzi huo ulikuwa unasubiriwa kwa siku nyingi na Kamati yetu kwani utamsaidia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika uimarishaji wa Utawala Bora hususan kwa kupunguziwa baadhi ya majukumu ya uwajibikaji kifedha na kuwezesha kuwepo kwa uwazi katika utekelezaji wa majukumu ya Afisi ya CAG.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati zetu mbili za Kuchunguza na Kudhibiti masuala ya kifedha, tunatanguliza pongezi zetu kwa Ndugu Said kwani tunatambua uwezo na uwajibikaji wake katika usimamizi wa fedha za Serikali na utendaji kiujumla, Kamati yetu inaamini jicho la Mheshimiwa Rais wetu limeenda kwa mtu sahihi na kwa wakati sahihi. Aidha, ni matumaini ya Kamati zetu kwamba uteuzi wake ni sawa na kumchukua samaki na kumuweka katika bahari hasa ukizingatia ni mtu mbobezi na mtaalamu wa masuala ya fedha na ukaguzi. Kwa maana hiyo tusubiri mengi mazuri atakayoyafanya kwa Afisi yake na Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC ilipitia Programu zote mbili za Afisi ya Mdhibiti zinazohusiana na Udhibiti na Ukaguzi wa Fedha na Rasilimali za Umma pamoja na Utawala na Uendeshaji wa Udhibiti na Ukaguzi ambapo katika utekelezaji wake, Kamati iligundua kasoro chache ambazo zinakwaza uwabikaji na utendaji wa Afisi ya Mdhibiti

na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na:

1) KUPANGIWA MAKADIRIO MAKUBWA KULIKO UWEZO WA MAKUSANYO WA VYANZO VYA AFISI YA CAG

**Mheshimiwa Spika,** katika kuyapitia makadirio ya makusanyo ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati ya PAC imebaini kwamba Afisi hiyo imepangiwa makadirio makubwa yasiyolingana na uwezo wa Afisi kwani kuna vyanzo viwili tu vinavyotokana na ada ya ukaguzi pamoja na chanzo kinachotokana na kodi ya matumizi ya ukumbi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imechunguza uwezo wa upatikanaji wa mapato wa vyanzo hivyo na kubaini kwamba kwa mwaka mmoja vyanzo hivyo vinaweza kukusanya jumla ya 270,000,000 na sio milioni 325,000,000 iliyopangwa na Wizara ya Fedha na Mipango sawa na ongezeko la asilimia 20 la uhalisia wa makusanyo ya Afisi ya CAG. Lakusahngaza zaidi Mheshimiwa Spika, mwaka jana Afisi hiyo ilipangiwa kukusanya shilingi milioni 250,000,000 ambapo hadi kufikia Machi, 2023, imekusanya shilingi 185,000,000.

**Mheshimiwa Spika,** kuwekwa makusanyo makubwa yanayotofautiana na uwezo halisi wa upatikanaji wa mapato kwa Afisi hii, kunaweza kuizorotesha kiutendaji hasa ukizingatia Afisi ya CAG inatekeleza majukumu yake sio tu kwa kufuata Sheria za nchi yetu bali pia inazingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali ilitaka kujua kwanini Wizara ya Fedha na Mipango ikapanga makusanyo makubwa ukilinganisha na uhalisia na kubaini kwamba Wizara ya Fedha na Mipango ilijumuisha na madeni ambayo Afisi ya CAG inayadai kutoka katika Taasisi mbali mbali za Serikali tangu mwaka 2019, jambo ambalo halipo sahihi katika utaratibu mzima wa upangaji makadirio wa kuyaingiza madeni ya nyuma ambayo hakuna uwezekano wa moja kwa moja wa kulipwa na kuipangia Taasisi iwe ndio makusanyo yake ya mwaka husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inaiomba Wizara ya Fedha na Mipango kukaa na kuangalia ipasavyo kiwango kikubwa cha makusanyo ambacho Afisi ya CAG imepangiwa ili kuiwezesha Afisi hiyo kuweza kufikia malengo yake ya makusanyo.

2) MADENI YANAYODAIWA NA AFISI YA CAG

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi wa Machi 2023, Afisi ya CAG haijafanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 65,000,000 ya mapato ya makusanyo iliyokadiriwa. Hali hiyo imetokana na ukweli kwamba kuna Taasisi za Serikali ambazo tayari zimeshafanyiwa ukaguzi lakini bado hazijalipa madeni yao, jambo ambalo linaipelekea Afisi kushindwa kufikiwa malengo yake iliyojipangia ya makusanyo.

**Mheshimiwa Spika,** lakushangaza, kuna Taasisi zenye madeni sugu ambazo hazijalipa madeni yao tangu mwaka 2019/2020, 2020/2021 na 2022/2023. Lakushangaza zaidi Mheshimiwa Spika, baadhi ya Taasisi hizo zina uwezo mkubwa wa kifedha wa kumudu kulipa malipo hayo ndani ya mwezi mmoja au miwili. Lakini hadi Kamati inapitia mapendekezo ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi hii, bado hazijaamua kulipa madeni ya ukaguzi wanayodaiwa na Afisi ya CAG.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu imegundua, jumla ya Afisi saba bado hazijalipa madeni yao ya ada ya ukaguzi kwa muda mrefu ni pamoja na Shirika la Bandari ambalo hadi Juni, 2021 linadaiwa milioni 17,600,000, Wakala wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumi hadi Juni, 2021 linadaiwa shilingi 7,000,000, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali hadi Juni, 2021 halijalipa shilingi 7,000,000, Mamlaka ya Usafiri Baharini hadi Juni halijalipa shilingi 8,800,000, Bodi ya Wasarifu wa Majengo hadi Juni, 2021 haijalipa shilingi shilingi 7,000,000 na ZAFICO ambapo hadi Juni, 2020 linadaiwa shilingi 6,000,000.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imeamua kuzitaja Taasisi hizi sio kwa lengo la kuziaibisha isipokuwa kuwaongezea nguvu Afisi ya CAG ili Taasisi hizo ziweze kuwajibika ipasavyo kwa kukamilisha malipo ya madeni wanayodaiwa hasa ukizingatia Afisi ya CAG imeshachukuwa juhudi kadhaa za kukumbushia malipo ya madeni hayo bila ya mafanikio yoyote ikiwemo kuwaandikia barua pamoja na kuzungumza nao.

3) UWASILISHAJI WA RIPOTI YA PAC ZAIDI YA MARA MOJA KWA MWAKA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imebaini kwamba kutokana na uchapaji kazi wa Afisi ya CAG uliotokana na juhudi za makusudi zilizofanywa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuwaongezea watendaji wakiwemo wataalamu wa fani tofauti za ukaguzi pamoja na vitendea kazi ikiwemo uwepo wa mfumo wa IFIMS, kumepelekea uwezo wa kiutendaji wa Afisi hii kuongezeka maradufu ukilinganisha na wakati uliopita.

**Mheshimiwa Spika,** wakati umefika sasa wa Kamati hizi za kifedha ambapo kwasasa ni Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) pamoja na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) kuruhusiwa kuongezewa muda wa utekelezaji wa kazi zake pamoja na kuwasilisha ripoti yake angalau kwa vipindi viwili kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imelipendekeza hilo kutokana na sababu kwamba ushauri na mapendekezo ya Kamati hizo yatatolewa ndani ya muda muafaka na wale wote

waliohusika na kadhia za upotevu na ubadhirifu wa fedha za umma wataweza kuchukuliwa hatua stahiki kwa wakati stahiki. Vile vile, Kamati zetu za kifedha zitapata muda wa kutosha kuzipitia, kuzifuatilia na kuzichunguza ipasavyo ripoti zote zitakazowasilishwa na CAG kwa wakati. Kwa mfano mwaka jana Kamati zako za Kifedha za PAC na LAAC hazijakamilisha kuzifanyia uchunguzi Ripoti zilizowasilishwa na CAG wakati hivi sasa Baraza lako Tukufu tayari limeshapokea Ripoti mpya saba ambazo zimeshawasilishwa hapa Barazani.

**Mheshimiwa Spika,** iwapo Ripoti mpya zitawasilishwa, itazifanya Kamati zako za kifedha iache kuzifanyia kazi Ripoti za mwaka jana na kushungulikia Ripoti mpya ambazo nazo si dhani kama Kamati zako zitamaliza kuzifanyia kazi kabla ya kuwasilishwa Ripoti nyengine za miaka ijayo.

**Mheshimiwa Spika,** iwapo hilo litaendelea kutokea litapelekea utumiaji mbaya wa fedha za Serikali pasi na Serikali kupata ushauri na mapendekezo ya Kamati katika uchukuliwaji hatua stahiki kwa watendaji wanaohusika.

## 4) NAIBU MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUWA AFISA MASUUL WA FUNGU LA AFISI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa miongozo ya kitaifa na kimataifa pamoja na Sheria zinazosimamia uendeshaji wa Afisi kama hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, inamtambua Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa ndie Afisa Masuul wa Afisi ya CAG.

**Mheshimiwa Spika,** kwa bahati mbaya, wakati Kamati yetu inapitia makadirio ya Mapato na matumizi ya Afisi hii, ilibaini kwamba bado Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ametambuliwa kuwa ndio Afisa Masuul jambo ambalo Kamati ya PAC imewaelekeza watendaji wa Idara ya Bajeti kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha wanarekebisha kasoro hizo ili kitabu cha makadirio kiweze kuendana na maelekezo ya miongozo ya kiutendaji ya Afisi za CAG duniani.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kueleza hotuba hii fupi inayohusiana na makadirio ya mapato na matumizi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yaliyoandaliwa kwa mashirikiano ya Wajumbe na Makatibu wa Kamati yetu. Kwa umuhimu wao, na kwa ruhusa yako, naomba sasa nichukue fursa hii kuwatambua Wajumbe na Makatibu kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Juma Ali Khatib - Mwenyekiti;
2. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Makamo Mwenyekiti;
3. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Mjumbe;
4. Mhe. Maryam Thani Juma - Mjumbe;
5. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman - Mjumbe;
6. Mhe. Sulubu Kidongo Amour - Mjumbe;

7. Ndg. Maryam Haji Ali - Katibu; na
8. Ndg. Said Khamis Ramadhan - Katibu.

**Mheshimiwa Spika,** Sitokuwa mwenye kutenda haki iwapo nitakamilisha hotuba yangu hii pasi na kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Mwalimu Haroun Ali Suleiman, kwa uwasilishwaji mwanana wa hotuba yake. Aidha, nawashukuru Viongozi na Watendaji wa Afisi ya CAG pamoja na Watendaji wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano wanayotupatia katika utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Kamati hususan ya kuchambua na kujadili bajeti ya Afisi hii ya CAG.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imeridhika na imeyakubali Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili waijadili, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae muiunge mkono bajeti hii, ili mipango mizuri iliyopangwa iweze kutelekelezwa kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati yangu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC), naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.



……………………
Mhe. Salha M. Mwinjuma,
**Kny: Mwenyekiti,**
**Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na**
**Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC),**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar.**